



Fifth EsF Assembly  
Hyderabad, India  
30 July-August 13, 2016

Montessori Education for Social Change  
Serving Humanity - Celebrating Solidarity

## 2016 EsF Assembly Daily Summary

### Friday, 5 August 2016

---

Washiriki wa mkutano WwM walipata nafasi leo yakutembelea maeneo mbalimbali. Basi zuri lililoandaliwa na chakula kilichoandaliwa kwa ajili ya safari ili kuwasaidia kundi la washiriki lililokuwa likitalii maeneo mbalimbali ya mkoa wa Hyderabad. Kituo cha kwanza kilikuwa Shule ya Pebble Creek Montessori ambayo ilianzishwa mwaka 2005 na kuendelezwa kakita elimu ya msingi mnamo mwaka 2008. Shule ilitoa ushirikiano kwa washiriki wa Mkutano kutembelea madarasa na kuangalia watoto wakifanya kazi. Wafanyakazi walikuwa na utayari wa kujibu maswali yaliyoulizwa na washiriki. Shule sasa inaendelea na ujenzi kwa ajili ya sekondari.

Katika kituo cha pili, Washiriki wa mkutano walitembelea kundi la washonaji wa jadi. Mbinu zilizotumika katika upakaji wa rangi kwa mikono za nyuzi za asili zilielezewa. Msanii aliyefanya upakaji wa rangi alionyesha sampuli ya kazi alizokwisha kuzifanya na rangi za asili alizozitumia. Ndani ya kiwanda washiriki wa mkutano waliweza kujionea mchakato wa kazi yenye maumivu makubwa ya jadi. Wale waliovutiwa ba kazi hiyo walipata nafasi yakununua vitambaa na kwenda navyo nyumbani.

Baada ya chakula cha mchana, kundi walifurahia kutembelea kituo kimojawapo kidogo cha Kiislamu cha Kimontessori kwa watoto wa miaka 3-6. Watoto waliimba nyimbo kwa washiriki wa Kongamano ana baadaye waliwpatiwa chai nzuri ya mchana. Kituo cha mwisho kwa siku kilikuwa kwenye soko lililoendeshwa na Shilparamam la Sanaa, Kazi za mikono na Utamaduni wa jamii, ambalo lilileta kwa pamoja kazi za mikono kutoka maeneo mbalimbali ya vijijini. Hii ilikuwa sehemu nzuri sana kwa kupata vitu vya ukumbusho kabla ya kurudi kwenye sehemu ya kupumzikia na kabla ya chakula.

---